TAMASHA LA KUMI NA MOJA LA ASASI ZA KIRAIA - ZANZIBAR

“Misingi ya Utawala Bora na Ustawi wa Asasi za Kiraia Zanzibar”

23 - 24 SEPTEMBA. 2017 - HOTELI YA OCEAN VIEW ZANZIBAR

MAELEZO KWA WASHIRIKI

YALIYOMO:

MAELEZO YA JUMLA: 3

KAMATI YA MAANDALIZI: 4

SALAMU - THE FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY: 5

SALAMU - ANGOZA: 6

HABARI KUHUSU ANGOZA:

a. UTANGULIZI: 7

b. MAADILI: 8

c. PROGRAMU: 8

MAELEZO YA TAMASHA: 9

ORODHA YA ASASI: 11

RATIBA YA TAMASHA: 15

MAELEZO YA JUMLA:

Imekuwa ni kawaida ya kila mwaka kwa ANGOZA chini ya ufadhili wa shirika la The Foundation for Civil Society kuwakutanisha wadau kwa kufanya utetezi katika masuala ya kisera wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia Midahalo na Maonyesho. Aidha kuzikutanisha Asasi katika Tamasha ambalo ni jukwaa la kujadiliana kwa pamoja, kujitathmini na kubainisha fursa na changamoto mbalimbali katika sekta hii ikilenga zaidi kufikia Mikakati ya Kitaifa ya MKUZA III na Dira 2020.

Kupitia Midahalo hiyo ya utetezi wa masuala ya Kisera imepelekea kutungwa, kufanyiwa mapitio na utekelezaji wa Sera na Sheria mbalimbali kama vile:-

- Sera ya Jumuiya za Kiraia ya mwaka 2009
- Sheria ya Serikali za Mitaa No. 7 ya mwaka 2014
- Sera ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014

Kupitia Sera na Sheria hizo ANGOZA imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi kwa njia za mafunzo, mikutano ya uhamasishaji, urushaji vipindi vya televisheni na redio na kutengeneza Sheria na Sera hizo kwa lugha nyepesi ambazo hufahamika kwa urahisi na wanajamii.

Masuala ya Utawala Bora na Ustawi wa Asasi za Kiraia ndio mjadala mkuu katika tamasha hili ambalo litakutanisha wanaharakati 120 kutoka Asasi za Kiraia, watumishi wa Serikali, vyama vya wafanyakazi, taasisi za elimu ya juu na waandishi wa habari watajadili kwa pamoja misingi ya Utawala Bora, Fursa na changamoto zilizopo katika utekelezaji wake.

Majadiliano baina ya Asasi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Masuala ya Kisera

KAMATI YA MAANDALIZI:

Kamati ya Maandalizi ni Kamati inayoratibu shughuli nzima ya Tamasha la 2017 yenye wajumbe kutoka Uongozi wa ANGOZA na baadhi ya Asasi wanachama. Kwa heshima kamati inapenda kuwakaribisha katika Tamasha la Kumi na Moja la Asasi za Kiraia.

Tamasha hili lina kauli mbiu ambayo itaamsha tafakuri ya kina katika kupata ufanisi wa utekelezaji wa misingi ya utawala Bora kwa upande wa Asasi za Kiraia, Serikali na hata mtu mmoja mmoja ngazi ya jamii, Wilaya hadi ngazi ya Taifa. Nchi yetu imelizingatia hilo kwa kuweka Wizara inayoshughulikia masuala ya Utawala Bora, Tume ya Haki za Binaadam,mifumo na taratibu za kiutawala na Sera ya Utawala Bora ambayo kwa sasa inafanyiwa mapitio na wadau wamekuwa wakishiriki katika mijadala ya Sera hiyo.

Tamasha hili limebeba mada mbalimbali zitakazowasilishwa na wataalamu wetu kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa mageuzi ya Utawala Bora, ushiriki, fursa na changamoto za kila sekta na jukumu la Asasi za Kiraia ikiwa ni wadau katika kutekeleza masuala ya Utawala Bora.

Kwa muktadha huo kauli mbiu ya Tamasha la mwaka 2017 ni:

“Misingi ya Utawala Bora na Ustawi wa Asasi za Kiraia Zanzibar”

ANGOZA imeweka dawati maalum wakati wa Tamasha, na hapo ndio sehemu yako ya kwanza kutembelea ukifika kwenye Tamasha kwa kupatiwa maelezo na vitu vyengine vinavyohusiana na tamasha vikiwemo kabrasha, T-shirt, Mkoba na Beji yako ambayo utapaswa kuivaa kipindi chote cha Tamasha. Tafadhali jisikie huru kuuliza masuala kwa wahusika wa dawati hilo ambao wako tayari na watafurahi kukusaidia.

Karibuni wanaharakati wote katika **Tamasha la Kumi na Moja la Asasi za Kiraia** Zanzibar.

Tunawatakia kila la Kheri.

Kamati ya Maandalizi.

SALAMU - THE FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY:

Foundation for Civil Society kwa kushirikiana na Mwavuli wa Asasi za Kiraia Zanzibar umeendelea kutekeleza mradi wa kuimarisha uwezo wa Asasi za Kiraia Zanzibar. Mradi huu wa miaka miwili umejikita katika kuimarisha stadi na uwezo wa Asasi katika kuleta ushawishi na mageuzi ya kisera kwa lengo la kuleta mabadiliko endelevu. Kupitia mradi huu AZAKi zimeongeza ujasiri na uhodari katika kubuni na kutekeleza miradi yenye kuleta mabadiliko ya kisera katika jamii. Mradi pia umewezesha kuimarika kwa umoja na mshikamano miongoni mwa Asasi za kiraia Zanzibar, kupitia mikutano ya tafakari ya mwezi ya mwenendo wa sekta ya AZAKi.

Asasi pia zimeweza kujumuika na kubuni miradi ya pamoja ya ushawishi wa será. Aidha tamasha la Asasi za kiraia la Mwaka jana 2016 lilileta kwa pamoja takribani viongozi wa Asasi 130 na wadau wa maendeleo ikiwemo serikali na wanazuoni, wajumbe wa tamasha walipata wasaa wa kujadili kwa kina ustawi wa mambo ya msingi katika kupelekea ustawi wa jamiii sambamba na kubaini maeneo yenye kuhitaji ushawishi wa kisera katika uendeshaji wa Asasi za kiraia Zanzibar.

Nichuke nafasi hii kuwapongeza sana Mwamvuli wa Asasi za Kiraia Zanzibar na Mshauri Mwelekezi wa Asasi Bi. Salma Maoulid kwa jitahada nzuri za kufanikisha mradi huu pamoja na kufanikisha Tamasha la Asasi za Kiraia la mwaka 2016. Pamoja na mafanikio na pongezi hizi, bado jitihadi zaidi zinahitajika katika kuimarisha sekta ya AZAKi Zanzibar. Utafiti uliofanywa na Foundation for Civil Society kwa kushirikiana na Shirika la ESRF (Economic and Social Research Foundation) mwaka 2016, umebaini changamoto kadhaa zinazoikabili sekta ya AZAKi Zanzibar, ikiwemo ukosekanaji wa mbinu endelevu za utunishaji wa mfuko wa rasilimali, uhaba wa vitendea kazi, upungufu wa umahiri pamoja na uhaba wa watendakazi. Kwa kuzingatia haya Foundation for Civil Society kwa kushirikiana na Washirika wake wa Maendeleo, umeongeza muda wa mradi kwa kupindi cha miaka miwili ijayo 2018 - 2019. Katika awamu hii mpya ya mradi jitihada zitaongezwa katika kuimarisha utekelezaji kwa vitendo wa stadi za ujuzi zinazopelekea ushawishi wa kisera sambamba na kuendeleza jitihada za kuimarisha ustawi wa sekta ya Asasi za Kiraia Zanzibar.

Mwisho, nawakaribisha sana wote katika Tamasha la Asasi za kiraia la mwaka huu, ambalo litatuwezesha kutafakari kwa kina misingi ya Utawala Bora na ustawi wa Asasi za Kiraia Zanzibar. Nichukue nafasi ya kipekee kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano wa karibu pamoja na ushiriki wao katika Matamasha ya Asasi za kiraia Zanzibar kwa kipindi chote kuanzia Tamasha la Kwanza hadi sasa Tamsha hili la kumi na moja.

Ahsanteni sana

SALAMU - ANGOZA:

Napenda kutoa shukurani za dhati kwa niaba ya Mwavuli wa Asasi za Kiraia ANGOZA kwa wadau wa Sekta ya AZAKi katika kuhakikisha kwamba malengo yetu tuliyojiwekea yanafikiwa kwa kuzingatia mipango ya kitaifa na Kimataifa kama MKUZA III, Dira 2020 na malengo endelevu ya kidunia (SDGs). Aidha napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa washirika wetu wa maendeleo The Foundation for civil society kwa msaada wa kitaalamu katika kutekeleza miradi na kugharamia miradi hiyo. The Foundation for civil society wamekuwa nasi kuhakikisha sekta ya AZAKi inaimarika.

Mwaka 2016 ANGOZA iliendesha tamasha lenye lengo ya kutathmini uwezo wa Sekta ya AZAKi, fursa na changamoto zinazoikabili na majukumu yake katika kuleta maendeleo. Tamasha ambalo liliongozwa na kauli mbiu ya **"Ustawi wa Zanzibar: Dhima ya Asasi za Kiraia".** Mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo, kuongezeka kwa ushirikiano baina ya Asasi za Kiraia na wadau wa maendeleo, hivi sasa Jumuiya Ulaya imetoa fursa kwa Asasi kuandika mapendekezo ya Miradi na kuifadhili,utekelezaji wa Utawala Bora ngazi ya Serikali za Mitaa umefanyiwa kazi vilevile uwezo wa kufanya utafiti wa huduma za kijamii umeongezeka.

Tamasha la mwaka huu 2017 lina lengo la kuwakutanisha wanaharakati wa Asasi na wadau wengine katika kutafakari, kujitathmini, kujifunza na kuweka mikakati ya misingi ya Utawala Bora ngazi ya Wilaya, Kitaifa na Kikanda na kuweza kuifanyia kazi ipasavyo, hivyo Kauli mbiu yetu ni **"Misingi ya Utawala Bora na Ustawi wa Asasi za Kiraia Zanzibar"** ambayo itajadiliwa kupitia mijadala mikuu na warsha maalum.

Nazishukuru na kuzipongeza Asasi za Kiraia kwa ushirikiano wao kwa kujitolea katika kufanikisha jitihada za kuwahudumia wananchi wetu kwa kushirikiana na Serikali katika kupambana na Umaskini, Kukuza uchumi, Demokrasia na Utawala Bora.

Ni matumaini yangu kwamba Asasi na wadau wengine tutaitumia fursa hii kujifunza, kujenga mitandao, kubadilishana uzoefu na kuimarisha mahusiano, tunataraji pia tamasha hili litakuwa chachu ya ukuaji wa Sekta ya AZAKi kwa kuwa lengo letu ni kuibua mijadala ambayo itapelekea ufanisi wa utekelezaji wa masuala ya Utawala Bora inayozingatia mifumo na taratibu za kisheria.

Asha Aboud Mzee

Mwenyekiti ANGOZA.

HABARI KUHUSU ANGOZA:

UTANGULIZI:

Mwavuli wa Asasi za Kiraia Zanzibar - ANGOZA ni taasisi ya kijamii, isiyofungamana na masuala yeyote ya kisiasa na isiyozalisha faida. ANGOZA ni mwavuli wa Kitaifa wa Asasi zisizo za Kiserikali ambazo zinajishughulisha na masuala mbalimbali ya maendeleo ya jamii. ANGOZA ilianzishwa mwaka 1993 chini ya sheria ya Ardhi No. 101 ya mwaka 1953 na kuandikishwa tena upya chini ya sheria No. 6 ya Jumuiya za Kiraia ya mwaka 1995.

ANGOZA inajukumu muhimu la kutetea ustawi wa Asasi za Kiraia, kuziwakilisha vyema katika kuleta umoja na mshikamano baina ya AZAKi na kufanya ushawishi na mabadiliko endelevu.

DIRA:

Kuwa na Asasi wanachama wenye Ari, Ufanisi na Uwajibikaji katika kuleta maendeleo endelevu na maisha bora kwa wazanzibari.

DHAMIRA:

Kuimarisha mitandao kwa kuijengea uwezo, kupashana habari, ushawishi na utetezi, utafiti, upangaji na usimamizi wa miradi ili kupambana na umaskini na kuimarisha Utawala Bora Zanzibar.

MALENGO:

Kwa kushirikiana na wanachama ANGOZA inalenga kuleta maendeleo endelevu ya Asasi za Kiraia ili kuimarisha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii na kuimarisha Utawala Bora kwa ustawi wa wazanzibari. Kwa kufanya hayo ANGOZA inalenga katika kuimarisha ushirikiano, kujenga ubia na mashirika na mitandao mingine yenye maoni yanayoshabihiana na ya ANGOZA.

MALENGO MAHSUSI:

- Kuratibu shughuli za AZAKi kwa nia ya kusimamia ubora na ufanisi wa shughuli zake.
- Kujenga uwezo wa AZAKi kwa kuongeza ufanisi na kuwa chanzo muhimu cha taarifa, ujuzi na maarifa.
- Kufanya ushawiishi na utetezi ili kujenga mazingira bora ya utendaji wa AZAKi
- Kuratibu na kuimarisha mshikamano na kujenga sauti ya pamoja kitaifa na kimataifa miongoni mwa makundi ya wanaharakati na AZAKi.
- Kuratibu na kuimarisha mshikamano kitaifa na kimataifa kati ya ANGOZA na Asasi nyengine.

WANACHAMA:

Asasi zilizosajiliwa na sheria No. 6 ya Jumuiya ya mwaka 1995 zina fursa za kuwa wanachama kwa kuwasilisha taarifa zao za usajili, katiba na kumbukumbu za makubalioano ya Jumuiya. ANGOZA ina jumuiya wanachama 230 ambao wanafanya kazi maeneo tofauti.

MAADILI:

ANGOZA inaamini katika Haki, Usawa, Ushirikishwaji, kupinga Ubaguzi, Kujitolea, Uwazi na Uwajibikaji.

PROGRAMU:

Katika kufikia malengo yake ANGOZA inatekeleza kazi zake kupitia programu zake za:

KUJENGA UWEZO:

Kupitia programu hii ANGOZA inatoa ujuzi, mbinu, na maarifa kupitia mafunzo mballimballi ya kiuongozi kwa wanachama wake kwa kuwajengea uwezo katika kusimamia majukumu yao katika jumuiya zao kwa ufanisi.

USHAWISHI / UTETEZI:

ANGOZA huaandaa matamasha, Midahalo na Maonyesho kwa watunga Sera ili kuweza kuzingatia matakwa ya jamii katika Sera kwa kutungwa, kufanyiwa mapitio na marekebisho ya Sheria mbalimbali. Na kujenga mahusiano ya karibu na watunga sera na watoa maamuzi.

TAFITI:

ANGOZA imejikita zaidi katika tafiti za huduma za jamii hasa utoaji na upatikanaji wa huduma za jamii kama Ufuatiliaji wa Rasimali za Umma (PETS) na Tathmini ya shirikishi ya Jamii katika Upatikanaji wa Huduma (PSDA).



UPASHANAJI HABARI:

ANGOZA inabadilishana taarifa na wanachama na wasio wanachama zinazohusiana na Asasi juu ya uandishi wa miradi, utafutaji wa fedha za kutekeleza miradi na ushiriki wa mikutano ya kupashana habari.

MAELEZO YA TAMASHA:

Hili ni Tamasha la mwaka la Asasi za Kiraia ambalo hukutanisha wadau mbalimbali kutoka Asasi za Kiraia, Serikali na Sekta Binafsi. Mada tofauti huwasilishwa, kujadiliwa na kuwekewa mikakati ya utekelezaji. Kwa mwaka huu wa 2017 Tamasha limejikita katika masuala ya Misingi ya Utawala Bora na mahusiano yake katika ustawi wa Asasi za Kiraia Zanzibar.

Kauli mbiu hii ya **"Misingi ya Utawala Bora na Ustawi wa Asasi za Kiraia Zanzibar"** inachochea hamasa za wananchi na Asasi kuwa tayari katika kuielewa na kuifanyia kazi kwa njia ya kubadilishana taarifa za msingi katika masuala mazima ya Utawala Bora pamoja na misingi yake ya Uwajibikaji, Uwazi, Ushirikishwaji, Usalama, Maadili ya viongozi wa Umma na Utendaji kazi wa Mihimili ya Dola. Na imekuja muda muafaka ambapo Serikali ipo katika mchakato wa kuifanyia mapitio Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011 na ugatuzi wa Madaraka kutoka Serikali kuu kwenda Serikali za Mitaa. Mikutano mbalimbali na wadau imekuwa ikiendelea na Asasi kwa upande wake inalizungumzia hili kwa kusisitiza na kuweka mkazo zaidi kwa Sera inayofanyiwa mapitio kuzingatia changamoto zilizopo na hatimaye kuja na Sera imara.

Tamasha hili linafanyika tarehe 23 na 24 Septemba, 2017 katika ukumbi wa Hoteli ya Ocean View uliopo kilimani Unguja na kufunguliwa rasmi tarehe 23 saa 03:00 asubuhi na **Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utawala Bora na Utumishi wa Umma Zanzibar. Na kufungwa tarehe 24 saa 10:00 Alasiri na Mheshimiwa **Moudline Cyrus Castico** Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto Zanzibar.

Lengo kuu

Kukuza uzingatiaji wa masuala ya Utawala Bora katika ugatuzi wa Madaraka, Haki za Binaadam, na mifumo ya usimamizi wa taratibu na sheria.

Malengo Mahsusi:

- Uwajibikaji wa majukumu na mazingatio ya misingi ya Utawala Bora kwa Asasi za Kiraia.
- Kukuza uelewa kwa Asasi juu ya viashiria vya Utawala Bora kwa kuzingatia Haki za Binaadam.
- Kuelimisha AZAKi juu ya ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda katika Wilaya na kujipanga katika ufuatiliaji wa matumizi ya Rasilimali za Umma.
- Asasi kuweza kujitathmini katika nyanja ya Utawala Bora ili kujua vipi AZAKi zinaakisi mifumo ya kisheria na changamoto za kiutawala.

Katika Tamasha hili jumla ya mada kumi zitawasilishwa na kujadiliwa kwa pamoja na washiriki ambazo zimegawika katika makundi mawili, Mada Kuu ambazo zitajadiliwa katika mijadala ya pamoja na kundi la pili ni mada zitakazojadiliwa katika warsha maalum ambapo washiriki watajadili katika makundi kwa siku ya kwanza na ya pili.

Mada kuu zitakazojadiliwa:

Mijadala	Mada
Kauli Mbiu: "Misingi ya Utawala Bora na Ustawi wa Asasi za Kiraia Zanzibar"	
Mada Kuu	"Namna Mageuzi yanavyoakisi masuala ya Utawala Bora na Uhusishaji wa Ustawi wa Asasi za Kiraia"
Uzingatiaji wa Misingi ya Utawala Bora Zanzibar	
Mjadala Mkuu	"Ugatuzi wa Madaraka Katika Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa na Misingi ya Utawala Bora"
Mjadala Mkuu	"Viashiria vya Utawala Bora na Uzingatiaji wa Haki za Binaadam (Hali ya Utawala Bora)"
Utawala Bora kama chachu ya ukuaji wa Sekta ya Asasi za Kiraia	
Mjadala Mkuu	"Asasi za Kiraia Zanzibar na Uzingatiaji wa Misingi ya Utawala Bora Zanzibar"
Mjadala Mkuu	"Mifumo na Taratibu za Kisheria na Changamoto za Kusimamia Utawala Bora"

Mijadala katika Warsha Maalum

Mijadala	Mada
Mada	"Maono ya Ugatuzi katika Sekta ya Elimu"
Mada	"Maono ya Ugatuzi katika Sekta ya Afya"
Mada	"Fursa za Ugatuzi kupitia huduma za Ugani"
Mada	"Utawala Bora na Mipango Dira ya Taifa (MKUZA III na Dira 2020)
Mada	"Mustakbali wa Uhuishaji wa Utawala Bora na Mapitio ya Sera.

ORODHA YA ASASI WASHIRIKI:

No.	Jina la Asasi	
Kundi linalowakilisha Mazingira		
1.	CODECOZ	Community Development and Conservation of Environment
2.	JAMABECO	Jambiani Marine and beach Conservation
3.	JECA	Jozani Environmental Conservation Association
4.	KIDIKE	Jukuiya ya Uhifadhi wa Mazingira na Popo
5.	MECA	Mkokotoni Environmental Conservation Association
6.	JUMAVUMA	Jumuiya ya Mazingira, Vitalu na Upandaji Miti Asilia
7.	VECA	Vitongoji Environmental conservation Association
8.	SEDCA	Jumuiya ya Uhifadhi wa Mazingira na Maendeleo Kusini Unguja
9.	JUHIMKO	Jumuiya ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe
10.	REZA	Renewable Energy Zanzibar Association
11.	WECOC	Wete Environmental Conservation Club
12.	ZACCA	Zanzibar Climate Change Alliance
13.	JUMAKA	Jumuiya ya Mazingira Kambini
14.	JUMUMI	Jumuiya ya Uhifadhi wa Mikoko na Kuendeleza Mali asili Micheweni
15.	JUKUNUM	Jumuiya ya Kufuga Nyuki na Mazingira
16.	JUMAWAPE	Jumuiya ya Maendeleo ya kushughulikia Mazingira Pemba
Kundi linalowakilisha Watu Wenye Ulemavu		
17.	JUWAUZA	Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar
18.	UWZ	Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar
19.	ZANAB	Zanzibar National Association for the Blind
Kundi linalowakilisha wakulima		
20.	ZAFFIDE	Zanzibar Farmers and Fishermen Development
21.	KOFDO	Jumuiya ya Maendeleo ya Wavuvi wa Kojani
22.	UWAMWIMA	Umoja wa Wakulima wa Matunda na Mbogamboga
23.	JUKAVIPE	Jumuiya ya Ustawishaji wa zao la Karafuu na Viungo Pemba
24.	OFA	Organic Farming Association
25.	JUWAKIZA	Jumuiya ya wakulima wa Kuendeleza kilimo cha kisasa Zanzibar
26.	JUWAwWE	Jumuiya ya Wafugaji Wila ya Wete
27.	MVIWATA	Mtandao wa vikundi vya wakulima Tanzania - Tawi la Zanzibar

28.	POFADEO	Poulirty Farmers Development Organization
29.	UWEMAJO	Umoja wa Wenye Mashamba Jozani
30.	MKEKIZA	Mtandao wa kutoa elimu ya wakulima Zanzibar - Tawi la Pemba
31.	JUVIMJA	Jumuiya ya Vitalu na Maendeleo ya Jamii
32.	MWAFIDO	Mwambe Fisherman Development Organization
33.	JUWAWAJE	Jumuiya ya Wakulima na Wafugaji Jendele
Kundi linalowakilisha vijana		
34.	ZYF	Zanzibar Youth Forum
35.	KIYEDO	Kidimni Youth Empowerment Development Organization
36.	SAO	Social Awareness Organization
37.	JUVIKUKA	Jumuiya ya Vijana ya Kupunguza Umaskini Zanzibar
38.	GAMYDA	Gamba and Mwoga Youth Development Association
39.	JMVT	Jumuiya ya Maendeleo Vijana Tumbe
40.	ZAYODEA	Zanzibar Youth Development Association
41.	KOYMOCC	Kojani Youth Mobilization Care Centre
42.	PIYDO	Pemba Investment Youth Development Organization
43.	ZCGF	Zanzibar Current Generation Forum
44.	JUVIEKA	Jumuiya ya Vijana Kaskazini ‘A’ Unguja
Kundi linalowakilisha Asasi za Elimu		
45.	TUSODA	Tunaweza Development Association
46.	ZPMO	Zanzibar Pre Madrassa Organization
47.	JUWASEZA	Jumuiya ya walimu wa Skuli za Sekondari Zanzibar
48.	PIRO	Pemba Island Relief Organization
49.	ISSO	Islamic Society Saves Organization
Kundi linalowakilisha Asasi za Afya		
50.	SWAZA	Saidia Wagonjwa wa Akili Zanzibar
51.	ZAIADA	Zanzibar Association of Information Against Drug Abuse and Alcohol
52.	WAMATA	Walio katika Mapambano na Aids Tanzania - Tawi la Pemba
53.	MIDECAC	Micheweni Islamic Development Environmental Conservation and Aids Control
54.	UMATI	Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania - Tawi la Zanzibar
55.	PEHECO	Pemba Herbalist Community
56.	JUWADAHIZ	Jumuiya ya Wachangiaji Damu wa Hiari - Zanzibar
57.	MISCO	Michewen Society Care Organization

58.	WTBS	Wakunga wa Jadi Wilaya ya Wete Pemba
59.	JUKAMKUM	Kuelimisha Athari za Madawa ya Kulevya VVUna Mimba za Umri Mdogo
Kundi linalowakilisha Haki za Binaadamu na Utawala Bora		
60.	ZAFELA	Zanzibar Female Lawyers Association
61.	TPIF	Tanzania Peace Initiative Foundation
62.	ANGOZA	Association of NGOs of Zanzibar
63.	ZLSC	Zanzibar Legal Service Centre
64.	JUWAZA	Jumuiya wa Wazee na Wastaafu Zanzibar
65.	NAHARAWANI	Association for Human Relief and Awareness for Women and Investments of Youths
66.	KUKHAWA	Kupunguza umasikini na kuboresha hali za wananchi
Kundi linalowakilisha Wataalamu		
67.	ZAMELSO	Zanzibar Association foe Medical Laboratory
68.	ZHOA	Zanzibar Health Officers Association
69.	ZAAA	Zanzibar Accountants And Auditors Association
70.	JUWALAZA	Jumuiya ya Wakalimani wa Lugha za Alama Zanzibar
71.	PPC	Pemba Press Club
Kundi linalowakilisha Asasi za Wajasiriamali		
72.	JOCDO	Jumuiya ya Mikopo na Maendeleo Jozani
73.	WEDTF	Women Entrepreneurs Development Trust Fund
74.	CHANGAMOTO	Jumuiya ya Changammoto
75.	AZASPO	Association of Zanzibar Salt for Processing Organization
Kundi linalowakilisha Asasi Wanawake na watoto		
76.	ZACA	Zanzibar association for Children Advancement
77.	ZASCO	Zanzibar adults, Street Children and Orphans
78.	JUWAKAP	Jumuiya ya wanawake mkoa wa Kasikazini Pemba
79.	MWASWD	Mwanyanya Women Association for Social Welfare development
80.	JUMWATU	Jumuiya ya Maendeleo ya Wanawake wa Tundauwa
81.	COWPZ	Catalyst Organization for Women Progress in Zanzibar
Kundi linalowakilisha CBO		
82.	WSS	White Star Society
83.	KIGUNDA	Jumuiya ya Maendeleo Kigunda
84.	MDS	Mkwajuni Development Society

85.	TUJIPE	Tumaini Jipya Pemba
86.	CHUMATO	Jumuiya ya Chambani Ukutini Matale na Tondooni
87.	TASOP	Tumbatu Association for Social Promotion
88.	RADEA	Rahaleo Development Association
89.	JUMACHO	Jumuiya ya Maendeleo Chokocho
90.	JUMWAKI	Jumuiya ya Maendeleo Wadi ya Kipange
91.	JUWAKIMABA	Jumuiya ya Wavuvi wa Kina Kirefu na Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari
92.	HIMACHA	Hifadhi ya Mazingira Chaani
93.	JUMATU	Jumuiya ya Maendeleo Tumbe
94.	KIDEO	Kiungoni Development Organization
95.	CHADESO	Chambani Development Society
96.	JUMAWAMA	Jumuiya ya Maendeleo ya Watu wa Mangapwani
97.	UWEMAJO	Umoja wa Wenye Mashamba Jozani
98.	J - MCHANGA	Jumuiya wa Wachimbaji Mchanga
Kundi linalowakilisha Taasisi za Serikali/ Mitandao / Mashirika		
99.	NORECSONET	North Region Civil Society Organization Network
100.	PACSO	Pemba Association for civil society
101.	ZGC	Zanzibar Gender Coalition
102.	PNYD	Pemba Network for Youth Development
103.	NOPACSO	North Pemba Alliance for Civil Society
104.	ZATUC	Zanzibar Trade Union Congress
105.	WBVM	Wakala wa Biashara na Mali
106.	WKSUUB	Wizara ya katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
107.	ZPC	Zanzibar Planning Commission
Kundi linalowakilisha Taasisi za Elimu ya Juu		
108.	SUZA	Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar
109.	ZCHS	Chuo cha Afya Zanzibar
110.	KATI	Chuo cha Kilimo Kizimbani Zanzibar

RATIBA YA TAMASHA:

Muda	Tukio	Mhusika
01:30 - 02:30	Kuwasili na Kujisajili	Kamati ya Maandalizi
02:30 - 03:30	MADA KUU: “Namna Mageuzi yanavyoakisi masuala ya Utawala Bora na Uhusishaji wa Ustawi wa Asasi za Kiraia”	Dr. Mohammed Makame Mhadhiri Chuo Kikuu Zanzibar
03:30 - 05:00	UFUNGUZI • Mrejesho wa tamasha lililopita 2016 • Uzinduzi wa ripoti ya Hali ya Asasi za kiraia Zanzibar • Kumkaribisha mwakilishi wa FCS • Kumkaribisha Mgeni Rasmi	Mwenyekiti - ANGOZA
	• Ufunguzi rasmi wa Tamasha	Mhe: Haroun Ali Suleiman Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
	• Neno la shukurani	Ndugu: Adil Mohammed Ali Mjumbe Kamati Tendaji - ANGOZA
05:00 - 05:30	**Chai**	**Wote**
MJADALA MKUU: “Uzingatiaji wa misingi ya utawala bora Zanzibar”		
05:30 - 07:00	MWONGOZAJI:	HAMZA RIJALI
	Mada ya kwanza: “Ugatuzi wa Madaraka katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Misingi ya Utawala Bora”.	Ndugu: Abdulrahman Mnoga Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
	Mada ya Pili: “Viashiria vya Utawala Bora na uzingatiaji wa haki za Binaadam” (Hali ya Utawala Bora)	Kamishna: Mohammed Tume ya Haki za Binaadam na Utawala Bora Zanzibar.
07:00 - 08:00	**Chakula cha Mchana**	**Wote**
WARSHA MAALUM: “Upeo wa Ugatuzi Kisekta”		
08:00 - 09:30	MWONGOZAJI	Ndugu: KHAMIS SAID – AKF
	WARSHA NO. 1 “Maono ya ugatuzi katika sekta ya elimu”	Ndugu: Masoud Mohamed Haji Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

		Amali Zanzibar
	MWONGOZAJI	Ndugu: KIDAWA RAMADHAN- ZACA
	WARSHA NO. 2 “Maono ya Ugatuzi katika sekta ya Afya”	Ndugu: Issa Abeid Mussa Wizara ya Afya
	MWONGOZAJI	Ndugu: Omar A. Mohammed
	WARSHA NO. 3 “Fursa za Ugatuzi kupitia huduma za ugani”	Ndugu: Abdullah Salum Wizara ya Kilimo
09:30 - 10:00	MREJESHO WA WARSHA MAALUM “Mafunzo na mazingatio Muhimu”	Waongozaji wa Warsha Maalum
10:00 - 11:00	Utawala	

SIKU YA PILI

Muda	**Tukio**	**mhusika**
MJADALA MKUU: **“ Utawala Bora kama chachu ya ukuaji wa Sekta ya Asasi za Kiraia”**		
01:30 - 02:30	Kuwasili na Kujisajili	Kamati ya Maandalizi
02:30 - 04:30	MWONGOZAJI:	Ndugu: SALMA HAJI SAADAT - UWZ
	Mada ya kwanza: “Asasi za Kiraia Zanzibar na uzingatiaji wa misingi ya Utawala Bora”	Ndugu: Hassan Vuai Idara ya Utawala Bora
	Mada ya pili: “Mifumo na taratibu za kisheria na Changamoto za kusimamia Utawala Bora	Ndugu: Salma Maoulid - Mshauri
04:30 - 05:00	**Chai**	**Wote**
WARSHA MAALUM: MIFUMO YA UTAWALA BORA		
Mwongozaji:	HASSAN KHAMIS JUMA	ANGOZA
05:00 - 06:30	WARSHA NO. 1 “Utawala Bora kama mpango Dira wa Taifa”(MKUZA III, Dira2020)	Kamishna Ahmed M. Haji Tume ya Mipango Zanzibar
	ASHA ABOUD MZEE	ANGOZA
	WARSHA NO. 2 “ Mustakbali wa uhuishaji wa Utawala Bora na mapitio ya Sera”	Ndugu: SAID – UTAWALA BORA
06:30 - 07:00	MREJESHO WA WARSHA NDOGO “Mafunzo na mazingatio muhimu”	Waongozaji wa Warsha Maalum

07:00 - 08:00	**Chakula cha Mchana**	**Sekreariet**
08:00 - 08:30	MREJESHO WA TAMASHA NA MIPANGO YA BAADAE	Mkurugenzi Mtendaji - ANGOZA
08:30 - 09:30	Mjadala wa wazi	Katibu Mkuu - ANGOZA
10:00 - 11:30	UFUNGAJI • Neno la shukurani • Kumkaribisha Mwakilishi wa FCS • Kumkaribisha Mgeni Rasmi	Katibu Mkuu - ANGOZA
	• Ufungaji	Mhe: Moudline Cyrus Castico Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto Z'bar
11:30 - 12:00	**Utawala**	**Kamati ya Maandalizi**

MAWASILIANO

Association of NGOs of Zanzibar - ANGOZA

S.L.P 4686 Zanzibar

Simu: +255 24 223 9325 / +255 773 306 684 / +255 776 497 514 / +255 777 457 413

Email: angozaznz@yahoo.co.uk or info@angoza.or.tz

Website: www.angoza.or.tz

Mtaa wa Mombasa Nyumba No. 22 Barabara ya Fumba